**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO**

# UFAFANUZI KUHUSU AMRI YA KIMA CHA CHINI CHA MSHAHARA KWA SEKTA BINAFSI

***Ndugu wanahabari;***

Mtakumbuka kuwa mwezi Oktoba, 2025, Waziri mwenye dhamana na masuala ya kazi alitangaza Amri ya Kima cha Chini cha Mshahara kwa Sekta Binafsi kupitia Gazeti la Serikali la tarehe 13 Oktoba, 2025. Amri hiyo imeanza kutumika tarehe 1 Januari, 2026. Aidha, kupitia taarifa aliyoitoa kwa umma tarehe 17 Oktoba, 2025 Waziri pamoja na mambo mengine, alieleza kuwa Kima cha Chini cha Mshahara kimeongezeka kwa wastani wa asilimia 33.4 kutoka wastani wa Shilingi 275,060/= hadi 358,322/=.

***Ndugu wanahabari;***

Ongezeko hili ni la wastani wa jumla ikilinganishwa na kima cha chini kilichotangazwa mwaka 2022 ambacho kimefikia ukomo wake tarehe 31 Disemba, 2025. Kwa msingi huo, niwatake Waajiri na Wafanyakazi wa Sekta Binafsi kuelewa kuwa viwango vya kima cha chini vimeainishwa kwa kuzingatia sekta kupitia Jedwali la Pili la Amri husika ambayo imegusa sekta mbalimbali ikiwemo kilimo, afya, mawasiliano, usafirishaji, hoteli, madini, biashara na viwanda, shule binafsi, huduma za ulinzi binafsi, nishati, uvuvi na huduma ya baharini, michezo na utamaduni pamoja na huduma nyinginezo.

***Ndugu wanahabari;***

Tunapoelekea kumaliza mwezi Januari, nitumie fursa hii kuwaelekeza Maafisa Kazi nchini kote kuendelea kutoa elimu kwa Wafanyakazi na Waajiri kuhusu Kima cha Chini cha Mshahara kilichotangazwa na utekelezaji wake. Aidha, nitoe wito kwa Waajiri na Wafanyakazi wote wa Sekta Binafsi nchini kuzingatia viwango vya chini vilivyowekwa na kushirikiana na Maafisa Kazi pamoja na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi ili kuendelea kupata elimu na ushauri kuhusu utekelezaji wa Amri hiyo.

***Ndugu wanahabari;***

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan itaendelea kushirikiana na Waajiri, Wafanyakazi pamoja na Vyama vyao kuhakikisha mazingira ya kazi na hali za Wafanyakazi zinaboreshwa na kusimamiwa ipasavyo ili kukuza Tija na Ustawi wa Wafanyakazi.

Ninawatakia utekelezaji mwema.

Deus Clement Sangu
**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, AJIRA NA MAHUSIANO**

**16 JANUARI, 2026**